**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. PHILIP ISDOR MPANGO, MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KATIKA UZINDUZI WA JENGO LA MAMA NA MTOTO, HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA SEKOU TOURE – MWANZA

**SEPTEMBA 2022**

- **Mheshimiwa Dkt. Godwin Molley (Mb.), Naibu Waziri wa Afya;**
- **Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wote mliopo hapa;**
- **Mheshimiwa Adam Kighoma Malima, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza;**
- **Dkt. Thomas Rutachonzibwa, Mganga Mkuu wa Mkoa;**
- **Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Mwanza;**
- **Dkt. Bahati Peter Msaki, Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Sekou Toure;**
- **Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya na Viongozi wote wa Chama na Serikali mlipo;**
- **Watumishi wote wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Sekou Toure;**
- **Viongozi wetu wa Dini;**
- **Ndugu Wananchi;**
- **Ndugu waandishi wa Habari;**
- **Wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana**

***Jamhuri ya Muungano wa Tanzania …***

Awali ya yote naungana na walionitangulia kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana siku ya leo. Nitumie nafasi hii pia kuwashukuru sana wana Mwanza kwa mapokezi mazuri sana, kwa kweli nimefarijika sana. **Asanteni**! Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, amenipa heshima kubwa kumwakilisha katika uzinduzi wa Jengo hili la Mama na Mtoto la Hospitali yetu hii ya Rufaa ya Mkoa wa Mwanza na amenituma niwasalimu na kuwahakikishia kuwa Serikali yake inaendelea kuzifanyia kazi changamoto zote zinazowakabili wakazi wa Mkoa wa huu wa Mwanza.

***Waheshimiwa Viongozi, Ndugu Wananchi, Mabibi na Mabwana;***

Uamuzi wa kujenga Jengo la Mama na Mtoto katika hospitali ya Sekou Toure, ulitokana na ukweli kwamba mahitaji ya huduma hizo katika Jiji la Mwanza ni makubwa. Hali kadhalika, mahitaji hayo ni makubwa katika Mikoa mingine hapa nchini. Serikali inaendelea kutenga fedha za kujenga na kuboresha miundombinu ya afya kote nchini ikiwa ni pamoja na kusogeza huduma hizo karibu na wananchi katika maeneo ya vijijini. Napenda kuwapongeza Wizara ya Afya na uongozi wa Mkoa wa Mwanza kwa kusimamia ujenzi wa Jengo la Mama na Mtoto katika Hospitali hii na kuhakikisha linakamilika kwa wakati na

kuanza kutumika. Kwetu sisi, ni jambo la faraja kuona tumepunguza sehemu ya changamoto iliyokuwa inawakabili wakaazi wa Jiji la Mwanza. Aidha, napenda kuwapongeza madaktari na wahudumu wa afya kote nchini kwa kazi kubwa wanayofanya kuwahudumia wagonjwa. Mnafanya kazi nzuri licha ya changamoto zilizopo kwenye maeneo yenu ya kazi. Nawaomba muendelea kujituma na kufanya kazi kwa upendo kuwahudumia wananchi. Aidha, mjiepushe na vitendo vinavyoharibu sifa njema ya tasnia ya utabibu ikiwa ni pamoja na kutozingatia maadili ya kazi. Serikali itaendelea kuboresha mazingira yenu ya kazi lakini pia tutaendelea kuchukua hatua za kisheria dhidi ya yeyote atakayebainika kujihusisha na vitendo viovu vinavyoendena kinyume na maadili yenu ya kazi.

***Waheshimiwa Viongozi, Ndugu Wananchi, Mabibi na Mabwana;***

Sote tutakubaliana kuwa ili mtoto apatikane, ni lazima kuwepo ushirikiano wa Baba na mama. Huduma za afya kwa mama na mtoto ni muhimu kwa sababu uzazi ni mwanzo wa uhai wa mwanadamu duniani. Ni muhimu kufamu kuwa, huduma hizi ni muhimu katika vipindi vyote vya mama mjamzito ikiwemo kabla mama hajapata ujauzito, wakati wa ujauzito, wakati wa kujifungua na maendeleo ya afya ya mama na mtoto baada ya kujifungua. Kwa ajili hiyo, ili afya ya mama na mtoto iimarike, ni lazima baba ashiriki katika upangaji wa mimba, ueleaji wa mimba, kujifungua na malezi ya mama na mtoto baada ya kujifungua. Hivyo basi, pamoja na kuwa Jengo hili ni maalum kwa mama na mtoto, elimu ya afya ya uzazi ni lazima itolewe kwa wazazi wote wawili ikiwa tunataka kufanikiwa kutoa huduma bora za afya kwa mama na mtoto.

Naomba nitoe rai kwa viongozi wote wa Serikali, dini mbalimbali na kwenu madaktari na wahudumu wa afya, kuhimiza akina baba kuhudhuria kliniki kila inapobidi kufanya hivyo ili kunusuru uhai wa mama na mtoto aliyeko tumboni wakati wa kipindi chote cha kulea mimba hadi mtoto anapozaliwa. Aidha, nitumie fursa hii kuwaomba wazazi kuzingatia maelekezo ya kitaalam yanayotolewa na madaktari na wahudumu wa afya ili kuepuka athari zinazoweza kutokana na uzazi ikiwemo vifo vya akinamama na watoto.

***Waheshimiwa Viongozi, Ndugu Wananchi, Mabibi na Mabwana;***

Kama nilivyotangulia kusema, huduma za afya ya mama na mtoto zinahusisha huduma za malezi ya mimba na malezi ya mtoto baada ya kujifungua. Kwa mujibu wa tafiti za kiafya, lishe bora katika kipindi cha siku elfu moja (1,000) za kwanza tangu mimba kutungwa ni muhimu sana kwa ukuaji wa ubongo na akili ya mtoto. Aidha, lishe bora kwa mama ni muhimu pia ili aweze kuwa na afya njema na kulea mimba na kuzalisha maziwa ya kutosha ya mtoto baada

ya kujifungua. Natambua kuwa madaktari na wahudumu wa afya mmekuwa mkitoa elimu ya lishe kwa mama na mtoto kabla na baada ya kujifungua.

Napenda, nitumie hadhara hii pia kuziomba taasisi mbalimbali na wadau wa lishe hapa nchini, kuunga mkono juhudi hizi za kutoa elimu ya lishe ili akina mama wawe na mimba salama na kuzaa watoto wenye afya njema. Hali kadhalika, niwaombe pia ndugu wananchi kuachana na imani potofu kuhusu matumizi ya baadhi ya vyakula na kuhakikisha mama na mtoto wanapata lishe bora kwa manufaa yetu binafsi na Taifa letu kwa ujumla. Mtoto akipata lishe bora anaepukana na magojwa ya mara kwa mara na hivyo kuepusha gharama ambazo zingetokana na matibabu. Vilevile, hatuna budi kuchukua hatua sasa, ili baada ya miaka kadhaa tuwe na Taifa lenye nguvukazi ya watu wenye uwezo mkubwa wa kufikiri na tija katika kazi za aina zote.

***Waheshimiwa Viongozi, Ndugu Wananchi, Mabibi na Mabwana;***

Upatikanaji wa huduma za afya hususan huduma bora za afya kwa mama na mtoto bado imeendelea kuwa ni changamoto licha ya jitihada za Serikali kuhakikisha huduma hizo zinapatikana kwa watanzania wote. Mahitaji ya huduma bora za afya kwa mama na mtoto hapa nchini bado ni makubwa ukilinganisha na miundombinu ya afya iliyopo na rasilimali zilizopo kujenga miundombinu zaidi.

Mojawapo ya changamoto za sekta ya afya ni gharama kubwa za matibabu. Aidha, hivi sasa Serikali inaandaa utaratibu mzuri ambao utakapokamilika utawezesha kila mwananchi kuwa na bima ya afya. Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote utawasilishwa katika kikao cha Bunge kinachoanza leo. Serikali tunaendelea kuhimiza matumizi ya bima katika huduma za afya ili kuwapunguzia watanzania mzigo wa gharama za matibabu. Hivyo, naitaka Wizara ya Afya iendelee kufanyia kazi changamoto mbalimbali zinazoikabili NHIF na kuhakikisha wanufaika wa bima hiyo wanapata huduma za afya bila kikwazo chochote.

***Waheshimiwa Viongozi, Ndugu Wananchi, Mabibi na Mabwana;***

Nafahamu changamoto nyingine inayoikabili sekta ya afya ni uhaba wa miundombinu na uchakavu wa baadhi ya miundombinu ya huduma za afya. Baadhi ya majengo ya hospitali zetu kongwe yanahitaji ukarabati ili yaendelee kutoa huduma bora za afya. Aidha, baadhi ya maeneo ya nchi yetu bado hayana miundombinu ya huduma za afya ya kutosha. Sote tutakubaliana kuwa kila mtanzania hata aliye kijijini ana haki ya kupata huduma bora za afya tena karibu na mahali anapoishi. Ujenzi wa jengo hili la Mama na Mtoto hapa Sekou Toure utaigharimu Serikali takriban Shilingi Bilioni 13 hadi

kukamilika kwake. Mahitaji ya Hospitali kama hii ni makubwa kwa kila mkoa hapa nchini. Hivyo, naomba kutumia fursa hii, kuitaka Menejimenti ya Hospitali hii, Wizara ya Afya na wananchi kwa ujumla kutunza miundombinu ya jengo hili ili yaweze kudumu na kuwahudumia wananchi kwa miaka mingi. Sambamba na hili, nawashukuru pia uongozi wa Hospitali yetu hii ya Rufaa kwa kuamua kuendelea kuboresha miundombinu ya hospitali na kujenga majengo mapya mengine ambayo yatakidhi uhitaji wa wananchi katika kutoa huduma bora za afya.

Aidha, naiagiza Wizara ya Afya iendelee kufanya ukarabati na matengenezo ya majengo ya hospitali yaliyochakaa kote nchini na kuzitunza vizuri hospitali zetu ili ziendelee kuwahudumia watanzania. Hali kadhalika, nimepokea ombi lenu la ujenzi wa jengo la dharura na ajali pamoja na ICU, namwagiza Waziri wa Afya alifanyie kazi ombi hilo ili wagonjwa na wananchi wa Mkoa wa Mwanza wapate huduma iliyo bora zaidi.

***Waheshimiwa Viongozi, Ndugu Wananchi, Mabibi na Mabwana;***

Kabla sijamaliza hotuba yangu, kupitia hadhara naomba kusisitiza kuhusu suala la uhifadhi wa mazingira. Nawapongeza wananchi wa Mwanza kwa kuwa na mwamko wa uhifadhi wa mazingira, kwa kupanda miti na kufanya usafi katika maeneo yetu. Ni vyema katika ujenzi wa miundombinu mbalimbali, ikiwemo majengo ya hospitali kam hii, uzingatie uboreshaji wa mazingira kwa kuhakikisha uwepo wa miti kama ya vivuli na matunda pamoja na kuzingatia usafi wa mazingira. Viongozi inapaswa tutoe elimu kwa jamii katika kuhakikisha maeneo ya hospitali yanakuwa safi ikiwa ni pamoja na ukusanyaji wa taka, kwa kuhakikisha tunakuwa na vifaa na teknolojia zinazofaa katika kukusanya taka na tuboreshe udhibiti wa taka ili kuzuia uchafuzi wa mazingira.

Hivi sasa dunia inakabiliwa na changamoto ya mabadiliko ya tabianchi, yanayosababishwa na tabiawatu ambayo athari zake zipo katika sekta mbalimbali. Hivyo, naomba nitumie fursa hii kutoa rai kwa wana Mwanza na wananchi wote kwa ujumla kuacha kukata miti ovyo, kuacha kuharibu vyanzo vya maji na maeneo oevu kupitia shughuli za kilimo na ufugaji usiozingatia sheria na kanuni za uhifadhi wa mazingira. Natoa wito muendelee kushiriki kikamilifu katika harakati za uhifadhi wa mazingira, pamoja na suala zima la usafi. Tupige vita vitendo vya uchafuzi wa mazingira katika maeneo yetu pamoja na haya ya hospitali. Tuyatunze mazingira yetu ili yatutunze!

***Waheshimiwa Viongozi, Ndugu Wananchi, Mabibi na Mabwana;***

Naomba nimalize hotuba yangu kwa kuipongeza sekta binafsi hususan katika huduma za afya kwa kuendelea kuunga mkono jitihada za Serikali kusogeza

huduma za afya karibu na wananchi. Hospitali na vituo vya afya vya mashirika ya dini na watu binafsi vimekuwa na mchango mkubwa katika kuboresha upatikanaji wa huduma za afya nchini. Naomba niwahakikishie kuwa, Serikali ya Awamu ya Sita inaendelea kuweka mazingira rafiki ya uwekezaji katika sekta ya afya na kuwakaribisha wawekezaji kuwekeza hapa nchini. Tukiunganisha nguvu kwa pamoja, naamini tutafanikiwa!

Baada ya kusema haya, napenda kutamka kuwa **Jengo la Huduma za Mama na Mtoto katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Sekou Toure - Mwanza limezinduliwa rasmi.**

**Mungu Ibariki Afrika**

**Mungu Ibariki Tanzania**

**Asanteni sana kwa kunisikiliza**.